JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA KWANZA

27 OKTOBA, 2026

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TANO

KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 27 OKTOBA, 2026

I. WIMBO WA TAIFA NA WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI:

II. DUA:

III. TAMKO LA AHADI YA UZALENDO KWA WABUNGE WOTE:

IV. TAARIFA YA SPIKA:

V. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

WAZIRI WA FEDHA:

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

VI. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

1. **MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Halmashauri ya Mji wa Korogwe itapandishwa hadhi kuwa Manispaa.

2. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (KILOLO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Barabara ya Idete – Kiwalamo – Kimala Wilayani Kilolo itatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya matengenezo makubwa.

3. MHESHIMIWA AMINA GOOD SAID (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali inamkakati gani wa kuhakikisha Vituo vya Afya vinakuwa na Wauguzi wa kutosha nchini kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

4. MHESHIMIWA IMAMU MTUMWA VUAI (MAGOMENI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji):-

Je, Serikali itahakikishaje Mfumo wa *e-delivery* unawezesha Bunge na Wananchi kupima utekelezaji wa malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

5. MHESHIMIWA MOSES LUDOVICO KAEGELE (NKASI KUSINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itabadilisha Mfumo wa kulipa Ada za Leseni za Uvuvi kutoka Dola kwenda Shilingi ili kuleta unafuu kwa Wavuvi wa Nkasi Kusini.

WIZARA YA KILIMO:

6. MHESHIMIWA ISACK JOSEPH COPRIANO (MONDULI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatimiza ahadi za Viongozi Wakuu wanazozitoa kila wanaposimama kwenye Mji wa Mto wa Mbu juu ya Ujenzi wa Soko la mazao ya Kilimo.

7. MHESHIMIWA PATALI SHIDA PATALI (MBEYA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itajenga Skimu za Uwagiliaji kwenye Tarafa za Isangati, Usongwe na Tembela – Mbeya Vijijini.

WIZARA YA MAJI:

8. MHESHIMIWA AMINA MUSSA MKUMBA (KIBITI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakamilisha Mradi wa uchimbaji wa Visima 10 katika Kata ya Kibiti - Jimbo la Kibiti.

WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:

9. MHESHIMIWA ASYA SHARIF OMAR (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kudhibiti uingizwaji wa vifaa vilivyotumika *(used)* ambavyo havina ubora na vimetumika kwa muda mrefu.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

10. MHESHIMIWA MWINYI JAMAL RAMADHANI (BUMBWINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali haioni haja ya kuleta Sheria Bungeni ya kutambua haki za Kidini na Kimila katika kusimamia mirathi.

11. MHESHIMIWA TINNAR ANDREW CHENGE (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali haioni umuhimu kufanya Marekebisho ya Sheria ya Mirathi ili mali za Mama wa Watoto waliozaliwa nje ya ndoa ziingizwe kwenye mirathi.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

12. MHESHIMIWA HAWA MCHAFU CHAKOMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, ipi kauli ya Serikali kuhusu matukio ya ubakaji yanayoendelea na kupelekea Wahanga kupata mimba katika mazingira hayo.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

13. MHESHIMIWA SHADYA HAJI OMARI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kushirikiana na

Mataifa ya Afrika na Vyombo vikubwa vya Habari kutumia AFCON 2027 kutangaza utalii wa Tanzania.

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

14. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (NSIMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga Mnara wa Mawasiliano katika Kata ya Ugalla, Kijiji cha Mnyamasi - Nsimbo.

WIZARA YA NISHATI:

15. MHESHIMIWA JUMA RAMADHAN MUSTAFA KAWAMBA (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itasambaza umeme katika Vijiji na Vitongoji vya Jimbo la Igalula ambavyo bado havina huduma hiyo.

WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

16. MHESHIMIWA JASMINE CHESCO NG'UMBI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kurejesha uhai wa Mchezo wa Mpira wa Pete ambao umedorora hapa nchini.

WIZARA YA UCHUKUZI:

17. MHESHIMIWA KASSIMU AMARI MBARAKA (TANGA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa Reli ya Kisasa kiwango cha SGR kutoka Tanga – Kilimanjaro – Arusha utaanza.

WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

18. MHESHIMIWA JESCA YUDA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:-

Je, lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Kitongoji

cha Chimlata – Kongwa waliopisha eneo la Jeshi lenye hekari 530.

WIZARA YA UJENZI:

19. MHESHIMIWA BAKARI BAKARI SHINGO (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itakarabati Barabara ya Nyerere kipande cha Pugu kwa Rais hadi Chanika ambacho kimeharibiwa na mvua.

VII. MAAZIMIO YA BUNGE:

Azimio la Bunge la Kumpongeza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa Kuridhia na Kuwezesha kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 153 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika Jijini Arusha kuanzia Tarehe 5 – 9 Oktoba, 2026.

VIII. KAMATI YA MIPANGO:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2027/2028.

DODOMA **BARAKA I. LEONARD**
27 OKTOBA, 2026 **KATIBU WA BUNGE**